**Maswali na Majibu**

1. Mungu aliwapa watu ahadi gani kabla waende matekani?
   *Kwamba baada ya miaka 70 watarudi kwa nchi yao.*
2. Nani walichukua Wayahudi mateka? Nani aliwaruhusu warudi?
   *Nebukadreza aliwachukua mateka. Koreshi aliwaruhusu kurudi.*
3. Nani aliwaongoza Wayahudi 42,000 kurudi kwa nchi ya Israeli?
   *Zerubabeli na Yoshua*.
4. Wayahudi walianza kujenga nini Yerusalemu?
   *Walianza kujenga Hekalu*.
5. Nani alitia Wayahudi moyo ili waendelee kujenga Hekalu?
   *Zekaria na Hagai waliwatia moyo wa kuendelea kujenga Hekalu.*
6. Kuhani gani aliwaongoza Wayahudi kurudi kwa nchi yao? *Ezra*
7. Mbona Ezra aliudhika sana? Alifanya nini?
   *Ezra aliudhika kwa sababu Wayahudi waliasi Mungu kwa kuoa wanawake wakafiri. Alirudisha watu Kwa Mungu.*
8. Mbona Nehemia aliudhika?
   *Alisikia kwamba kuta za Yerusalemu zimebomoka.*
9. Nehemia alifanya nini?
   *Aliuliza mfalme ampe ruhusa ili aende Yerusalemu. Aliwaongoza watu kujenga kuta za Yerusalemu.*
10. Kuta zilichukuwa muda gani kujenga.
    *Zilichukuwa muda wa siku 52. Kila mtu alisaidia kujenga.*

## Mistari ya kukariri

Ezra 1:2 – 3 Nehemia 4:21 1 Wakorintho 15:58

## Mazungumzo

Wayahudi walisaidiana kujenga kuta hata kama maadui walijaribu kuwavunja moyo. Zungumza juu ya nini itakayokuvunja moyo. Tunaweza kusaidiana namna gani pamoja kufanyia Mungu kazi?

## Kuandika

Hawa watu wafuatao walikuwa nani? Walifanya nini? Zerubabeli na Yoshua; Hagai na Zekaria; Ezra; Nehemia.

# Masomo ya watoto wakubwa wa CBM

## Somo la 28 Ezra na Nehemia

**SOMA Ezra 1:1 – 8; 3:8 – 13; 4:1 – 5 na 24; 5:1 – 2; 7:1 – 10; 10:1 – 5**
**Nehemia 1:2 – 4; 2:1 – 9 na 11 – 13; 4:13 – 23; 6:15 – 16**

**SOMO**

Kwa somo lililopita tulisoma vile Mungu alipowapa watu wake wa Yuda ahadi ya tumaini. Kabla watu hawa hawajachukuliwa mateka kwa nchi ya Babeli, Mungu aliwaahidi kwamba atawarudisha kwa nchi yao tena. Mungu alisema watakuwa mateka kwa miaka 70. Halafu atawarudisha kwa nchi yao tena, Yerusalemu na Hekalu zitajengwa. Walipokuwa utumwani walitazamia sana huu wakati wa kurudi kwao.

Mfalme Nebukadreza alichukua watu wa Yuda mateka mpaka Babeli katika mwaka wa 606 kabla ya Kristo. Katika mwaka wa 536 kabla ya Kristo, yaani miaka 70 kamili, mfalme Koreshi aliwapiga Wakaldayo na kutoa amri kwamba Wayahudi warudi kwa nchi yao na wajenge Hekalu. Ahadi ya Mungu ilitimizwa kikamilifu.

Zaidi ya Wayahudi (watu wa Yuda) 42,000 walitaka kurudi kwa nchi yao ya Israeli. Lakini Wayahudi wengine hawakutaka kurudi. Walitaka kubaki Babeli. Wayahudi waliobaki Babeli waliwapa wale walioenda nyumbani zawadi ya dhahabu na fedha ili iwasaidie kujenga hekalu. Mfalme Koreshi aliwapa vyombo vyote vya dhahabu na fedha vyenye mfalme Nebukadreza alichukua kutoka kwa Hekalu.

Zerubabeli na Yoshua waliongoza karibu Waisraeli 42,000 kwenda kwa nchi ya Israeli. Walienda na dhahabu na fedha zote kutengenezea hekalu. Wayahudi wengi walizaliwa Babeli. Hawakuwa wameona nchi yenye Mungu aliwapa. Kila mtu alikuwa amefurahi kwenda kuishi kwa nchi ya Israeli.

Watu walikaa karibu na Yerusalemu, wakijenga Hekalu. Koreshi alikuwa amewapa pesa ya kuwasaidia kufanya hiyo kazi. Wakati msingi wa Hekalu ulipokwisha, walikuwa na sherehe ya kipekee ya shukurani ili wafurahi kwa sababu Hekalu ilikuwa inajengwa Yerusalemu tena.

Wakafiri walioishi kule walitaka kusaidia Wayahudi kujenga Hekalu. Wayahudi walikumbuka amri ya Mungu kwamba wao ni taifa la watu waliotengwa kuabudu Mungu. Hawakutakiwa kuchanganyika na wakafiri. Hao wakafiri walikasirika na kuanza kuvunja Wayahudi myoyo. Hekalu haikujengwa tena kwa miaka 16.

Mungu alituma manabii wawili, Hagai na Zekaria kuwapa watu moyo ya kuendelea kujenga Hekalu ili wamalize. Kazi ya kujenga Hekalu ilianza tena. Mwishowe Hekalu ilimalizika kujengwa na watu wakawa na sherehe kubwa ya shukurani kwa Hekalu.

Hekalu ya Mungu ilijengwa. Lakini wakafiri waliendelea kuvunja Wayahudi moyo. Mwishowe Wayahudi walisahau Mungu na hawakutii amri zake tena.

Ezra alikuwa kuhani wa imani. Aliishi Babeli. Miaka 60 baada ya Wayahudi kujenga Hekalu, Ezra aliamua kwenda Yerusalemu kuabudu Mungu kwa hiyo Hekalu. Ezra aliuliza Atarshasta mfalme wa Uajemi ruhusa ili aende aishi kwa nchi ya Israeli. Mfalme alikubali. Tena mfalme alimwambia akipenda angewachukua Waisraeli waliotaka kwenda Israeli.

Kulikuwa bado na Waisraeli wengi Babeli na walitaka kwenda kwa nchi yao ya Israeli. Mfalme alimpa Ezra zawadi nyingi za dhahabu na fedha za kutumia kwa Hekalu. Alimfanya Ezra kuwa gavana wa Yerusalemu. Ezra na Waisraeli walianza safari kutoka Babeli na wakafika Yerusalemu. Walishukuru Mungu na kupeleka dhahabu na fedha kwa Hekalu na kuabudu Mungu kule.


Ezra alikundua kwamba watu walikuwa wamesahau Mungu na waliasi amri zake. Waliungana na wakafiri wenye hawakujua Mungu. Walioa wanawake wakafiri. Ezra alikasirika sana. Hawa watu wa Mungu walichukuliwa mateka kwa ajili ya kutomtii Mungu. Mungu alitimiza ahadi yake kwao na akawarudisha kwa nchi yao - na sasa wamemuasi tena kwa kutomtii.

Ezra aliwaita Wayahudi wote Yerusalemu na akawafunza vile wanatakiwa waabudu Mungu. Watu wote waliahidi kumtii Mungu tena. Ezra alikaa Yerusalemu. Alikuwa na kazi kubwa ya kugeuza watu wamrudie Mungu. Ezra alikeuza watu kutoka kwa mambo ya wakafiri. Aliwageuza waabudu Mungu kwa ukweli. Aliwafundisha wakae kama watu wa Mungu wateule.



Nehemia alikuwa mnyweshaji wa Atarshasta, mfalme wa Uajemi. Siku moja alipata barua kutoka Yerusalemu. Ilisema kwamba kuta za Yerusalemu bado zimebomoka. Hazikuwa zimejengwa. Mafungu ya mawe yalifunika barabara na milango za kuta zilikuwa zimechomwa. Wayahudi walikuwa na maadui wengi na hawakuwa na kinga yoyote. Walikuwa kwa hatari sana kwa sababu hawakuwa na kinga yoyote kutoka kwa maadui wao. Nehemia aliudhika sana. Aliuliza mfalme ampe ruhusa aende Yerusalemu ili azijenge kuta tena. Mfalme alipea Nehemia ruhusa na pesa ya kutumia kujenga kuta. Nehemia alienda na Wayahudi wengine wengi sana waliotaka kwenda kwa nchi yao.

Nehemia alipofika Yerusalemu alizunguka kuta zote kwa punda ili aangalie kazi inayotakiwa kufanywa. Alizungumza na wakubwa wa Wayahudi. Walikubali kujenga kuta. Watu wote wa Yerusalemu walikubali kujenga kuta tena. Walifanya kwa vikundi vidogo. Wote walifanya kazi vizuri tena kwa bidii. Walifanya kazi pamoja, wake, waume, tajiri na maskini. Wengine walifanya zaidi ya wengine lakini hakukuwa na manun'guniko. Walikuwa na imani kwa Mungu na walijua atawazuia kutoka kwa maadui na watafanya kazi vizuri.



Maadui hawakufurahi, kwa hivyo walijaribu kuwazuia wasijenge. Lakini Wayahudi hawakuacha kujenga. Waliweka walinzi na tarumbeta ili wawaadharishe kama kuna adui. Wengine walifanya kazi wakiwa na upanga wakujizuia ikiwa watashambuliwa. Waliamini Mungu na wakafanya kazi kwa bidii.

Mungu alisaidia Wayahudi. Baada ya siku 52 tu, walimaliza kujenga kuta. Kuta za Yerusalemu zikawa za nguvu. Watu walisifu Mungu kwa sababu sasa wangeishi kwa amani.

Nehemia alikuwa kiongozi wa nguvu. Wakati mambo yalikuwa magumu, aliomba Mungu. Nehemia aliheshimu Mungu kila mara. Hakuogopa maadui. Alijua Mungu atasaidia. Nehemia alisaidia Wayahudi kujenga kuta za Yerusalemu ili waishi salama.